## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI JANUARI, 2026 NA MWELEKEO KWA MWEZI FEBRUARI, 2026.

**Dondoo za tathmini ya Januari, 2026 na mwelekeo wa Februari, 2026:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Januari, 2026 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Februari, 2026 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Januari, 2026 baadhi ya maeneo nchini yalipata mvua pamoja ngurumo, hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo machache.


ii. Hali ya joto iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo hususani nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani.

iii. Katika kipindi cha mwezi Februari 2026, mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka ikiwa ni muendelezo wa mvua za Msimu. Hata hivyo, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2026.

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2026 baadhi ya maeneo nchini yalipata vipindi vya mvua iliyoambatana na ngurumo, hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo machache. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 84.0 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Tabora, ikifuatiwa na milimita 63.0 katika kituo cha Tumbi (Mkoa wa Tabora), vyote vikipimwa mnamo tarehe 28 Januari, 2026. Vituo vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1. Kwa upande mwingine, vipindi vya joto viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 36.5 °C kilirekodiwa katika kituo cha Kilimanjaro mnamo tarehe 24 Januari, 2026.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 50 au zaidi katika mwezi Januari, 2026

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI FEBRUARI, 2026

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la chini kidogo ya wastani. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi, karibu na Pwani ya Afrika mashariki, linatarajiwa kuwa la, wakati eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani pamoja na mikoa ya jirani. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la wastani. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kudhoofika na kusababisha Ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia kusini mwa nchi.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2026

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2026 mvua za Msimu zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kuendelea hususan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa hususan wiki ya kwanza na ya pili.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI MACHI, 2026

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2026 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo yanayopta msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za Masika 2026 zinatarajiwa kuanza katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, hali ya joto inatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

## 2.4 USHAURI

Mvua za Msimu zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Februari, 2026 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*